
# Miongozo Bora ya Kuchukua Picha Zinazokubalika za Wanyama Jamii ya Nyani (primata)

Chapisho la Kikundi cha Wataalamu wa wanyama jamii Nyani Cha IUCN – kitengo cha mahusiano kati ya Binadamu na Nyani

Siân Waters, Joanna M Setchell, Laëtitia Maréchal, Felicity Oram, Janette Wallis & Susan M Cheyne

Na michango kutoka: Brooke Aldrich, Sherrie Alexander, Liana Chua, Tara Clarke, Malene Friis Hansen, Carolyn Jost-Robinson, Kimberley Hockings, Marni LaFleur, Lucy Radford, Erin Riley, Amanda Webber

## Utangulizi



Picha mgando (photo) au picha jongefu (video) (hapa zitajulikana kama taswira) zinaweza kuteka hisia za mamilioni ya watu juu ya uhifadhi na ustawi wa wanyama jamii ya nyani (hapa watajulikana kama nyani[1]). Hata hivyo , ikiwa maudhui ya picha/taswira hayafai, hayaeleweki, au hayapo, watu wanaweza kupata hitimisho potovu juu ya maudhui ya picha hizo. Mahitimisho haya yasiyokuwa sahihi yanaweza kuwa na matokeo hasi yasiyotarajiwa, kwa ustawi na uhifadhi wa wanyama jamii ya nyani (Aldrich 2018; Wallis 2018; Norconk *et al.* 2019). Athari za Usambazaji wa picha zisizokuwa na maudhui ya kufaa ni jambo la wasiwasi kwenye mitandao ya kijamii.

Katika nchi nyingi, nyani wanakamatwa kutoka msituni/porini kinyume cha sheria na kutumiwa kama zana za burudani katika picha kukuza utalii (Osterberg & Nekaris 2015; LaFleur *et al.* 2019; Norconk *et al.* 2019). Nyani wakubwa mara nyingi huuwawa ili kupata nyani wachanga/wadogo wa kutumiwa kama zana za burudani. Meno ya nyani yanaweza kuong'olewa ili kuwazuia kuuma. Nyani binafsi katika picha anaweza/wanaweza kuwa katika dhiki iliyokithiri sana. Kwa mfano, nyani watembeao nyakati za usiku tu kama vile slow lorises, huathiriwa sanana mwanga wa mchana na ule wa kurunzi wakati wanapotumiwa kama zana (props) katika picha (Nekaris *et al.* 2015). Watalii na wataalam wahamiaji mara nyingi huwanunua nyani hawa, na kuwafuga kama wanyama wa mapambo au kwa matumaini ya 'kuwaokoa' (Bergin *et al.* 2019; Osterberg & Nekaris 2015; LaFleur pers. obs.; Setchell pers. obs.). Zaidi ya hayo, kote katika nchi wanakopatikana na wasikopatikana nyani, wafanyabiashara wasio waaminifu huzalisha wanyama wa porini 'wa kigeni', ikiwamo sokwe wakubwa, kama zana za picha (Aldrich 2018). Mara tu wanyama hawa wanapokua wakubwa sana au kupata nguvu kiasi cha kushindwa kuwadhibiti, wanatupwa au kuhifadhiwa kwenye mabohari. Wanyama hawa mara nyingi huhifadhiwa katika mazingira duni ambayo jamii inaweza isijue au isijali (Agoramoorthy & Hsu 2005; Reuter & Schaefer 2016).

Wale wote ambao wanaufahamu juu ya nyani, watu kama vile wataalamu na wanafunzi wa utaalamu wa nyani, wahifadhi, wafanyikazi wa utunzaji wa wanyama, wajitolea katika bustani za wanyama, vituo vya uokoaji na vilevya kutunza wanyama, wafanyikazi wa serikali, na waelekezi wa watalii (kwa ujumla wao

---

Katika chapisho hili, neno 'nyani' linajumuisha aina zote za wanyama wanaofananishwa na binadamu na wala sio nyani (baboon) pekee. Kwa lugha ya Kiingereza neno 'Nyani', linalinganishwa na 'primates' katika chapisho hili.

hapa wakijulikana kama wajumbe) wana jukumu muhimu la kufikisha ujumbe sahihi kuhusu nyani. Kwa namna ile ile, ni muhimu pia wafadihili, watangazaji maarufu wa uhifadhi, waigizaji mashuhuri wa filamu na watangazaji mashuhuri wa televisheni, maafisa wa serikali na watayarishaji wa habari katika vyombo vya habari kuiga tabia inayofaa wanapohusiana na nyani. Mwisho wa yote, mafanikio ya ufikishaji ujumbe juu ya nyani yanategemea na namna gani ujumbe umepokelea na sio malengo/madhumuni ya Mjumbe.

Hapa chini, tunaelezea ni kwanini wajumbe tuliowataja hapo juu wafikirie upya matumizi yetu ya picha hasa zilitulizopiga karibu sana au tukiwa tumebeba nyani. Kwa hitimisho tunatoa miongozo itakayo punguza Gharama za matumizi ya taswira za nyani, ustawi wao na uhifadhi wao indani na nje ya pori.

## Athari za picha za watu wakiwa karibu sana na nyani

### Picha za watu wakiwa na nyani hubadili ufahamu wa jamii juu ya nyani

Picha katika mitandao ya jamii zikimuonesha binadamu amebeba nyani huketa athari hasi katika mtazamo wa jamii juu ya nyani (Ross *et al.* 2011; Nekaris *et al.* 2013; Leighty *et al.* 2015; Clarke *et al.* 2019). Picha ya binadamu akiwa amembeba au yuko karibu kabisa na nyani huleta matazamo usio sahihi kuwa kumgusa nyani hakuna hatari yoyote kimwili, hakuhatarishi afya ya binadamu au nyani, na kuwa nyani anaweza kuwa mnyama mzuri wa mapambo.. Tabia hizi zinaweza kusababisha watu kuona nyani kama vyanzo vya burudani tu, na kwa hivyo kudharau thamani yao kibioanuwai (biodiversity) na hali yao ya kutishiwa, ambayo inaweza kudhoofisha juhudi za uhifadhi haswa katika nchi ambazo nyani hupatikana(range countries) (Ross *et al.* 2008; Schroepfer *et al*. 2011; Leighty *et al.* 2015, Morrow *et al*. 2017; Aldrich 2018).

### Picha za watu wakiwa karibu sana na nyani zinaweza kuwa chanzo cha tafsiri tofauti katika tamaduni mbalimbali

Wakati baadhi ya tamaduni zimejitenga na asili na zinajitahidi kuweka toafuti dhabiti kati ya "binadamu" na "asili" au "wanyama por" , zingine nyingi hazifanyi hivyo, na watu sio lazima wawachukulie nyani kama wanyama "pori", haswa katika nchi ambazo nyani hupatikama(Aldrich 2018). Tunaweza kutarajia tafsiri ya picha kutofautiana kutokana jinsi watu wanavyo husiana na kuingiliana na nyani.. Kwa mfano, mtazamo juu ya nyani hutofautiana sana kati ya wakaazi wa vijijini na mijini (Franquesa-Soler & Serio Silva 2017; Ceballos-Mago & Chivers 2010). Tofauti hii ya mtazamo, inamaanisha kuwa ujumbe tunaotaka kuwasilisha na picha kutoka kwa mtazamo wa tamaduni moja au eneo moja hauwezi kuwa ujumbe utakao pokelewa na watu wa tamaduni au eneo jingine.

### Picha za wajumbe wakiwa na nyani zinaweza kushawishi umma/jamii kutaka picha zao wenyewe wakiwa karibu na nyani

Picha za madaktari wa mifugo, watunzaji wa wanyama, watangazaji wa vipindi vya wanyama pori, watu mashuhuri, watu wanaojitolea na watalii wakikumbatia au kulisha nyani kwenye vituo vya ukarabati huleta hamu ka umma na jamii kwa ujumla kufanyia hivyo hivyo. Watu kupata picha mgando za wao karibu na wanyama pori (ikiwa ni pamoja na nyani) bila kuwa na kizuizi chochote kati yao , imekuwa njia maarufu ya kupata, kusambaza na kuhalalisha uzoefu wa kusafiri (Shutt 2014). Picha kama hizo zinadhoofisha juhudi za wenyeji kupambana na ujangili, ufugaji wa wanyama kwa mapambo, jumbe za uhifadhi kwa kuonyesha muingiliano halisi kati ya binadamu na nyani ambao vituo vya uokoaji, NGO's na Wakala wanajaribu kuzipinga. gando. Zaidi ya hayo, picha m za wataalam wa nyani (primatologists) wakitunza nyani zinaweza kuchochea hasira za jamii za wenyeji, ambao wakati mwingine huhisi waifadhi wanajali wanyama sana kuliko watu (Meijaard & Sheil 2008; Waters et al. 2018).

## Hitimisho

**Kama watu wanaohusika na ustawi an uhifadhi wa nyani, tuna jukumu la kuzingatia athari za moja kwa moja na zile zisizo za moja kwa moja za kuchapisha picha zetu tukiwa karibu na nyani** (Wallis 2018). Katika vyombo vya habari maarufu, picha hizi za watu wakiwa na nyani zinzpunguza mtazamo sahihi wa jamii juu ya nyani, huongeza uwezekano wa kutokuelewana kwa tamaduni, huongeza mwingiliano usiofaa na nyani ambao unaweza kupunguza juhudi za ukarabati na ustawi wa nyani, na hupunguza juhudi za uhifadhi wa nyani katika mazingira yote. Athari mbaya za kuchapisha picha kama hizo zinaweza kuzidi athari nzuri, ni lazima tutumie kanuni aa tahadhari (precautionary principle), ikizingatiwa kiwango cha shida ya kutoweka kwa nyani.

Kwa ufupi, **kama wajumbe wa nyani tunaojielwa, tuna jukumu la kutokutuma katika mitandao ya kijamii picha zetu tukiwa karibu sana na nyani kwa sababu zinaweza sambazwa kwa urahisi kinyume na maudhui na kueweka vibaya.** Hii pia inatuhusisha sisi ambao tunafundisha, kuwasilisha katikamikutano, hufanya kazi kwenye vyombo vya habari/mitandao, na kuongeza maarifa juu ya uhifadhi wa nyani. Inatumika kwa kila mtu anayefanya kazi na, au kwa niaba ya, nyani, lakini haswa ni jukumu kwa sisi ambao tunajulikana kwa kazi zetu na nyani kwa sababu ya uwezo wetu wa kushawishi mtazamo wa umma/jamii kuhusu nyani.

Tunatoa miongozo itakayo punguza Gharama za matumizi ya taswira za nyani, ustawi wao na uhifadhi wao ndani na nje ya pori.

## Miongozo bora ya picha zinazohusisha za nyani

- Kuhakikisha wewe pamoja na / au shirika/taasis lako mna kanuni za mwenendo kuhusu usambazaji wa picha unaofanywa na wafanyakazi, wanafunzi na watu wanaojitolea. Pale inapofaa, hakikisha idara zaza masokona uhusiano wa umma au watu wa mawasiliano wanaojitolea wanafahamishwa kikamilifu kuhusu ya kanuni hizo.
- Wale ambao hawana udhibit wowote wa picha zao, kama vile watu mashuhuri ambao picha zao zimekuwa mtandaoni kwa muda, wanapaswa kuchapisha picha zingine na kuelezea kwanini picha halisi hazifai. Pia wana nafasi ya kutoa taarifa kwa umma kuelezea msimamo wao wa sasa.
- Kuza elimu kwa kuelezea katika tovuti yako au ya shirika/taasisi yako, machapisho, mawasilisho, mipango na ziara elekezi juu maswala yanayohusiana na picha za watu walio karibu na nyani kwa uhifadhi na ustawi wa nyani.
- Pale inapofaa, onyesha tabia inayofaa kwa kupiga picha watu wakiwa nje ya vyumba vya nyani waliofungiwa (isipokuwa kama nyani wanafugwa lakini wako mahali huru), badala ya ndani.
- Usichapishe picha za nyani wakiwa mikononi mwa mlezi. Badilisha picha hizi na picha za nyani akiwa peke yake au akiwa na wenzake.
- Usichapishe picha za nyani wakilishwa kwa mkono, wakicheza au kushirikiana moja kwa moja na walezi, wajitolea au wafadhili isipokuwa binadamu wakiwa wamevalia vifaa vya kibinafsi vya kujikinga.
- Hakikisha kwa zile picha zinazotumwa/kuchapishwa hadharani katika picha hizo kuna umbali wa mita 7 /futi 23, kati ya mtu na.
- Katika picha zinazo tangaza taaluma ya juu ya nyani "primatology" kama tahsusi "profession", hakikisha maudhui yake yako wazi kwa kujumuisha barakoa, darubini, daftari (notepad), au vifaa sawa na hivyo kwenye picha na ueleze maudhui yake.

## Marejeo


Agoramoorthy G & Hsu MJ. 2005. Use of nonhuman primates in entertainment in Southeast Asia. *Journal of Applied Animal Welfare Science* 8:141-149.

Aldrich BC. 2018. The use of primate actors in feature films 1990-2013. *Anthrozoos* 31:5-21.

Bergin D, Atoussi S & Waters S. 2018. Online trade of Barbary macaques *Macaca sylvanus* in Morocco and Algeria. *Biodiversity and Conservation* 27:531-534.

Ceballos-Mago N & Chivers DJ. 2010. Local knowledge and perceptions of pet primates and wild Margarita capuchins on Isla de Margarita and Isla de Coche in Venezuela. *Endangered Species Research* 13:63-72.

Clarke TA, Reuter KE, LaFleur M & Schaefer MS. 2019. A viral video and pet lemurs on Twitter. *PLoS ONE* 14(1): e0208577.

Franquesa-Soler M & Serio-Silva JC. 2017. Through the eyes of children: Drawings as an evaluation tool for children's understanding about Endangered Mexican primates. *American Journal of Primatology* 79: DOI.10.1002/ajp.22723.

LaFleur M, Clarke TA, Reuter KE, Schaefer MS & terHorst C. 2019. Illegal trade of wild-captured *Lemur catta* within Madagascar. *Folia Primatologica* 90:199-214.

Leighty KA, Valuska AJ, Grand AP, Bettinger TL, Mellen JD, Ross SR, Boyle P & Ogden JJ. 2015. Impact of visual context on public perceptions of non-human primate performers. *PLoS ONE* e0118487.

Morrow KS, Jameson KA & Trinidad JS. 2017. Primates in film. In *The International Encyclopaedia of Primatology* (eds M Bezanson, KC MacKinnon, E Riley, CJ Campbell, KAI Nekaris, A Estrada, AF Di Fiore, S Ross, LE Jones-Engel, B Thierry, RW Sussman, C Sanz, J Loudon, S Elton & A Fuentes). DOI:10.1002/9781119179313.wbprim0350

Meijaard E & Sheil D. 2008. Cuddly animals don't persuade poor people to back conservation. *Nature* 454:159. https://www.nature.com/articles/454159b.pdf

Nekaris KAI, Musing L, Vazquez AG & Donati G. 2015. Is tickling torture? Assessing welfare towards slow lorises (*Nycticebus* spp.) within Web 2.0 videos. *Folia Primatologica* 86:534-51.

Nekaris KAI, Campbell N, Coggins TG, Rode EJ, Nijman V. 2013. Tickled to death analysing public perceptions of "cute" videos of threatened species (slow lorises – *Nycticebus* spp.) on Web 2.0 sites. *PLoS ONE* 8(7):e69215.

Norconk MA, Atsalis S, Tully, G, Santillan AM, Waters S, Knott CD, Ross SR, Shanee S & Stiles D. 2020. Reducing the primate pet trade: Actions for primatologists. *American Journal of Primatology* DOI.org/10.1002/ajp.23079.

Osterberg P & Nekaris KAI. 2015. The use of animals as photo props to attract tourists in Thailand: A case study of the slow loris (*Nycticebus* spp.). *Traffic Bulletin* 27:13-18.

Reuter KE & Schaefer MS. 2016. Captive conditions of pet lemurs in Madagascar. *Folia Primatologica* 87:48-63.

Ross SR, Lukas KE, Lonsdorf EV, Stoinski TS, Hare B, Shumaker R & Goodall J. 2008. Inappropriate use and portrayal of chimpanzees. *Science* 319:1487 DOI 10.1126/science.1154490.

Ross SR, Vreeman VM, Lonsdorf EV. 2011. Specific image characteristics influence attitudes about chimpanzee conservation and use as pets. *PLoS ONE* 6:e22050.

Schroepfer KK, Rosati AG, Chartrand T & Hare B. 2011. Use of "entertainment" chimpanzees in commercials distorts public perception regarding their conservation status. *PLoS ONE* 6:e26048.

Shutt K. 2014. An interdisciplinary risk assessment of gorilla ecotourism. PhD, Durham University. Available at http://etheses.dur.ac.uk/10586/

Wallis J. 2018. The role of tourism in securing a sustainable existence for primates. In *Primatology, Biocultural Diversity and Sustainable Development in Tropical Forests.* UNESCO.

Waters S, Watson T, Bell S & Setchell JM. 2018. Communicating for conservation: circumventing conflict with communities over domestic dog ownership, North Morocco. *European journal of Wildlife Research* 64:69 doi: 10.1007/s10344-018-1230-x.


## Shukrani


Tunawashukuru sana, Wakfu wa Ouwehand Zoo, Uholanzi kwa msaada wao kwa Siân Waters katika uundaji wa miongozo hii. Shukrani ziwaendee Pravind Segaran, UMS/ Pongo Alliance, Sabah, Malaysia kwa michoro na Janette Wallis kwa mpangilio. Tunawashukuru wanachama/ wajumbe wa Halmashauri Kuu ya PSG na Linda May wa Wakfu wa Arcus kwa maoni juu ya toleo la mwanzo la miongozo. Laëtitia Marechal agependa kushukuru Mradi wa Barbary Macque, Chuo Kikuu cha Lincoln, Uingereza na Hifadhi ya Taifa ya Ifrane, Morocco.. Kwa habari zaidi, tembelea tovuti yetu www.human-primate-interactions.org.


OUWEHAND ZOO FOUNDATION